THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

021 **KISWAHILI**
(Kwa Watahiniwa walioko na Wasiokuwa Shuleni)

MUDA: Saa 3 ***Alhamisi asubuhi 11/10/2007***

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, B, C, D, na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu E. Swali la **12** ni la lazima.

3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org

Mtihani huu na mitihani mingine yanapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

SEHEMU A (alama 10)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kando ya namba ya swali.

   Nisubiri! Nisubiri nini? Sikupewa talaka. Nilitelekezwa. Jani linapeperushwa lakini hakuna mkono wowote unaothubutu kuliokota, kama vile ambavyo angesema nyanya yangu.

   Hata hivyo niliishi. Niliyajua matatizo ya usafiri yaliyokuwepo. Wanangu walikwenda shuleni kwa taabu lakini walivumilia na kuchekelea. Siku moja nikamsikia dada akiwashauri. "Hasa! Msimwambie mama jinsi watu wanavyobanana mwenye magari wakati wa kwenda na kurudi kazini".

   Nililia kwa furaha iliyochanganyika na huzuni. Nilifurahi kwa vile nilipendwa na wanangu na nilihuzunika kwa vile sikuwa na uwezo wa kuikabili hali halisi iliyokuwepo. Kwa hiyo nilikueleza bila kukuficha hali hiyo ya kuhuzunisha ya maisha yetu. Wakati ambapo bibi mama-mkwe alikuwa akizitembelea pembe zote za mji akitumia gari la Modu, na Binetuu alikuwa akitamba katika barabara zote akiendesha gari la aina ya Alfa Romeo, mara jekundu mara jeupe.

   Sitasahau kamwe jamala uliyonifanyia wewe, dada yangu. Wala sitasahau kamwe furaha na mshangao nilioupata wakati ambapo muuzaji wa magari ya aina ya Fiat aliponiita na kuniambia nichague gari nililotaka, na kwamba wewe ungegharimia kila kitu. Wanangu walishangilia kwa furaha walipotambua kwamba mahangaiko yao yalikuwa karibu kumalizika, mahangaiko wayapatayo wanafunzi wengi sana kila siku.

   Katika urafiki, mna upendo mkuu usiojulikana. Huwa unakomaa wakati wa matatizo. Lakini ukali uliozidi mno huua upendo. Urafiki hukaa imara katika nyakati zinazochosha na kuudhi na kuwatenganisha waliooana. Ama kwa hakika katika urafiki mna upendo uliolenga juu kabisa kusikojulikana. Wewe sonara ulijinyima na ukaweza kunisaidia wakati wa dhiki.

   Nikajifunza kuendesha na nikautawala woga wangu. Hii nafasi ndogo iliyoko kati ya usukani na kiti cha mbele ikawa yangu. Ninapokanyaga klachi mwendo unaongezeka. Nikikanyaga breki mwendo unapungua, na ninapotaka kwenda kasi nakanyaga akselereta. Nilijivunia akselereta. Nilipoikanyaga kidogo tu gari ilichanganya mwendo mkali. Miguu yangu ikajifunza kuchezecheza juu ya hizo pedali. Wakati nilipokuwa nimekata tamaa kabisa nilikuwa najisemea mwenyewe: "Kwa nini Binetuu aendeshe gari na siyo mimi? Tena niliwaza." Nisimdanganye Aisatu! Niliishinda hiyo vita ya mishipa ya fahamu na ya kujishinda binafsi. Niliipata leseni ya kuendesha na nilikufahamisha.

   Nilikueleza, na sasa je? Wanangu wakiwa wamestarehe kwenye kiti cha nyuma ya gari yangu aina ya Fiat 125, rangi ya maziwa, ambayo ulinileta wanaweza kumwangalia kwa dharau yule mke mwenzangu.

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

Maswali

(i) Mwandishi wa habari hii ana matatizo ya
A kupewa talaka na mumewe
B umaskini uliokithiri
C kutelekezwa na mumewe
D kutokuwa na usafiri
E kuwa na watoto wengi.

(ii) Binetuu ni
A rafiki yake mwandishi
B bibi mkwe wake mwandishi
C mke mwenzie mwandishi
D hawana uhusiano wowote
E jirani wa mwandishi.

(iii) Mwandishi anaposema “katika urafiki mna upendo mkuu … unakomaa wakati wa matatizo”, anamaanisha kuwa
A akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli
B rafiki wa kweli ni yule anayekupenda wakati wa dhiki tu
C kila shetani na mbuyu wake
D huruma ya kweli inapatikana wakati wa dhiki
E rafiki ni yule mwenye upendo wa chati.

(iv) Nyanya kama lilivyotumiwa na mwandishi maana yake ni
A tunda linaloungwa kwenye mboga
B rafiki mzee
C mama wa mzazi wako
D ajuza
E yote si kweli.

(v) Kulingana na habari hii kuna vitu vitatu muhimu vinavyotumika wakati wa kuendesha gari. Navyo ni:
A Usukani, breki na klachi
B Kiti cha dereva, klachi na akselereta
C Pedali, klachi na breki
D Klachi, akselereta na breki
E Akselereta na breki.

(vi) Neno “jamala” kama ilivyotumiwa na mwandishi linamaanisha
A wema wako
B juhudi zako
C rehema zako
D upendo wako
E upole wako.

(vii) Kulingana na habari hii Modu ni
A jina la mume wa mwandishi
B aina ya gari
C halijulikani maana yake
D majibu yote si kweli
E ni rafiki wa sonara.

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

(viii) Rafiki yake mwandishi kazi yake ni
A sonara
B mfanyabiashara
C muuza magari
D afisa
E dereva.

(ix) Sifa za watoto wa mwandishi kulingana na habari hii ni
A wenye upendo, huruma, wavumilivu na wapole
B wavumilivu na wenye furaha wakati wote
C wakaidi na wanaocheka ovyo
D wakaidi kwa majirani na marafiki
E sifa zote hizo wanazo.

(x) Mwandishi anazungumzia matatizo yanayowakumba wanawake
A katika jamii
B wasio na upendo
C waliotelekezwa na waume zao
D walioachiwa watoto kuwalea peke yao
E wote wenye ndoa.

2. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha andika ufupisho wa maneno 60 kuhusu habari hiyo.

Vijana popote duniani ni tegemeo la taifa. Kupuuza malezi ya vijana ni sawa na kupuuza uhai wa taifa. Leo hii tukitazama mwelekeo wa malezi ya watoto wetu, ipo hali ya kutatanisha sana. Sasa hivi malezi ya watoto hasa katika jumuiya yetu hapa Tanzania, yamekuwa na ugumu wa pekee.

Baadhi ya vijana wetu wamejiingiza katika mambo ya aibu, mfano ulevi, uvutaji bangi, mambo ya ngono na vitendo vingine viovu. Sasa hivi baadhi yao hawana aibu tena na wanayumba maishani. Wengine wanapenda maisha ya starehe, njia za kujipatia mali haraka haraka na mengine mengi ya kusikitisha.

Tukumbuke kwamba hawa ndio wataiongoza nchi wakati wazee wao watakapomaliza muda wao wa kuishi hapa duniani. Lakini hebu tujiulize swali moja. Ni nani alaumiwe? Je tuwalaumu watoto? Tuwalaumu wazazi au nani?

Mambo ya burudani yalikuwepo tangu zamani lakini yalikuwa na mipaka yake. Mathalani ilikuwa ni mwiko kwa vijana wa kike kutembea peke yao, walitembea katika vikundi.

Tendo la kuzaa nje ya ndoa lilikuwa likilaumiwa vikali na ilikuwa ni aibu kwa binti yeyote kukumbwa na balaa kama hilo.

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

SEHEMU B (alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

UTUMIZI WA LUGHA

3. Chagua kifungu cha maneno kutoka **orodha B** kinachotoa maelezo sahihi ya maneno/neno katika **orodha A**. Andika herufi ya jibu sahihi kando ya namba ya kipengele cha swali katika kijitabu chako cha kujibia.

Orodha A		**Orodha B**	
(i)	Nyanya	A	Irabu
		B	Shina
(ii)	a, e, i, o, u	C	Irabu/ fonimu
		D	Shina/mzizi
(iii)	Starehe	E	Sentensi
		F	Sentensi shurutia
(iv)	Angewahi angenikuta	G	Thelathini
		H	Ishirini na tano
(v)	Idadi ya fonimu za Kiswahili	I	Nomino
		J	Nomino/Tata

4. Katika kila moja ya sentensi zifuatzo onesha kosa la kisarufi kisha andika sentensi hiyo kwa usahihi:
   (a) Kiboko kinaogelea.
   (b) Arusi ya kaka yenu zitakuwa Disemba 2006.
   (c) Mwaka huu mvua zinanyesha sana.
   (d) Tafadhali nikope shilingi elfu kumi nitakurudishia kesho.

5. Andika insha yenye maneno mia **moja (100)** kuhusu moja ya mada zifuatazo:
   (a) Maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2005.
   (b) Upimaji wa virusi vya Ukimwi.
   (c) Mwenda tezi na omo marejeo ngamani.

SEHEMU C (alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

SARUFI

6. Tunga tungo yenye vipashio vifuatavyo
   (a) Nomino + Kishazi tegemezi + Prediketa + Shamirisho.
   (b) Kiima hapa + Prediketa + Chagizo.
   (c) Kirai nomino + Kishazi huru + Kishazi tegemezi.

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

7. Eleza dhima ya kiambishi “ni” kilichopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:
   (a) Alinisaidia.
   (b) Wajumbe wapo mkutanoni.
   (c) Wakubalieni.
   (d) Yeye ni mvivu.
   (e) Nina kalamu.

8. Bainisha kauli **tano (5)** za vitenzi na kila kauli itungie sentensi moja.

9. Kwa kutumia mifano ya sentensi eleza dhima **tano (5)** za mofimu “ku”.

SEHEMU D (alama 10)

Jibu swali la 10

HISTORIA YA LUGHA

10. Wakati wa ukoloni, Kiswahili kilienea zaidi Tanzania kuliko Kenya na Uganda. Taja sababu **tano (5)** zilizosababisha hali hiyo.

SEHEMU E (alama 40)

Jibu maswali **mawili (2)** katika sehemu hii. Swali la **12** ni lazima.

FASIHI

11. Fafanua fani na maudhui ya methali zifuatazo:
   (a) Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
   (b) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
   (c) Mchumia juani hulia kivulini.
   (d) Kipenda roho hula nyama mbichi.
   (e) Haba na haba hujaza kibaba.

12. “Mwandishi wa fasihi ni mchunguzi wa jamii ambaye huyaweka wazi maovu mbalimbali”. Jadili jinsi kazi za washairi **wawili** kati ya hao walioorodheshwa zilivyosadifu kauli hii.

13. “Matendo yasiyo na utu hujadiliwa na wasanii”. Thibitisha kauli hii kwa kutumia riwaya **mbili (2)** kati ya hizo zilizoorodheshwa.

14. Kwa kutumia tamthiliya **mbili (2)** kati ya hizo zilizoorodheshwa, jadili jinsi kazi za wasanii hao zilivyochangia katika ujenzi wa jamii.

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

Orodha ya Vitabu

Ushairi

Diwani ya Mloka	…….	C. Mloka (B.P.)
Malenga Wapya	…….	TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya Chekacheka	…….	T.A. Mvungi (EP & DLTD)

Riwaya

Kusadikika	…….	S. Robert (E.P.)
Watoto wa Mama N'tilie	…….	E. Mbogo (H.P.)
Kiu ya Haki	…….	Z. Mwanga (R.P.)

Tamthiliya

Mfalme Juha	…….	F. Topan (DUP)
Ngoswe - Penzi Kitovu cha Uzembe	……..	E. Semzaba (ESC)
Kilio Chetu	…….	Medical Aid Foundation (TPH)

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org